**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**Kenya Primary School Education Assessment**

# KISWAHILI
# LUGHA

## Gredi ya 6
### Muda: Saa 1

**<u>MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)</u>**

1. Umepewa kijitabu hiki cha Kiswahili na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30.

2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.

4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

   **NAMBA YAKO YA TATHMINI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMO**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.

6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.

7. Kwa kila swali 1 - 30 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu sahihi.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**
**Katika kijitabu cha maswali:**
**28.** Maneno katika jedwali hili yanastahili kuwa katika hali ya umoja pekee. Chagua jibu lenye maneno **yasiyo** katika hali ya umoja.

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | yai | dirisha | chandarua |
| B | uso | msusi | mwiko |
| C | ufagio | kiti | mswaki |
| D | kuni | vifutio | matunda |

Jibu sahihi ni D.

**Katika karatasi ya majibu:**
**28** [A] [B] [C] ~~[D]~~


9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.

10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**
*© 2022 The Kenya National Examinations Council*

**Swali la 1 hadi la 5**

*Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.*





*(Katiku na Solo wamekutana njiani.)*

**Solo:** Masalkheri Katiku?

**Katiku:** Akheri Solo. Habari za muda sahibu?

**Solo:** Njema. (*Akiyaangalia mavazi yake*.) Umetoka wapi?

**Katiku:** Nimetoka kwenye mazoezi ya mchezo wa kuigiza.

**Solo:** Hakika unapenda drama.

**Katiku:** Ndiyo. Drama inakuza ubunifu, mawasiliano na ushirikiano. Isitoshe, inaburudisha. Inaweza pia kukupa kipato maishani.

**Solo:** Kipato? Kumbe michezo ya kuigiza ina manufaa mengi hivi?

**Katiku:** Ndiyo, Solo. Si hayo tu. Drama pia hukuza uwezo wa kufikiria kwa kina na kutatua matatizo.

**Solo:** Aha! Sasa nimepata mwanga zaidi. Asante kwa kunielimisha.

**Katiku:** Karibu. Nawe unapenda mchezo upi?

**Solo:** Ninapenda mchezo wa chesi.

**Katiku:** *(Kwa mshangao)* Chesi? Nilifikiri ungetaja kandanda, jugwe au hoki !

**Solo:** *(Akitabasamu)* Ni mchezo mzuri. Unajua kuwa mchezo huu pia hunoa akili ?

**Katiku :** Aha! Sikuyafahamu hayo. Asante Solo.

**Solo:** Karibu. Sote tumeelimishana. Hakika elimu ni bahari!

**Katiku:** Kweli mwandani wangu. Kwaheri!

**Solo:** Kwaheri ya kuonana. *(Wote wanaondoka.)*

1. Badala ya masalkheri, solo pia angesema, ___________?
   A. hujambo
   B. umeamkaje
   C. shikamoo
   D. salama

2. Ni neno lipi la adabu alilotumia Solo katika mazungumzo haya?
   A. kumbe
   B. hakika
   C. asante
   D. aha

3. Sentensi zifuatazo zimetumiwa katika mazungumzo haya. Ni sentensi ipi inayoonyesha kuwa Katiku anakubaliana na alichosema Solo?
   A Nimetoka kwenye mazoezi ya mchezo wa kuigiza.
   B. Inaweza pia kukupa kipato maishani.
   C. Drama pia hukuza uwezo wa kufikiria kwa kina
   D. Kweli mwandani wangu. Kwaheri

4. Je, ungeyasikiliza mazungumzo ya Katiku na Solo, ungejifunza nini?
   A. Ni sharti ushiriki katika michezo ya kuigiza ili utambulike.
   B. Ni muhimu kubadilishana mawazo kuhusu mambo tunayoyajua.
   C. Kufikiria kuhusu michezo kunapunguza matatizo.
   D. Kufahamu aina zote za mchezo kunamletea mtu fahari.

5. Neno lingine ambalo lina maana sawa na **sahibu** ni:
   A. rafiki
   B. ndugu
   C. jirani
   D. binamu

**Swali la 6 hadi la 8**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

**KIJIJI CHA FANAKA**

Eneo la Jitegemee limo kaskazini mwa Kaunti ya Kambini. Jitegemee ina vijiji vitano. Fanaka ndicho kijiji kidogo zaidi hapo Jitegemee. Ni kijiji ambacho huwavutia na kuwashangaza wengi.

Wanakijiji wa Fanaka ni wenye bidii ya mchwa. Mtu anapotembelea Fanaka alfajiri hukutana na misafara ya watu ; wake kwa waume, wazee kwa vijana. Wao huwa wanaenda kutafuta riziki. Wapo wanaobeba vibuyu na mitungi, wanaenda kutafuta maji mtoni au kwenye vibanda vya maji. Wengine hubeba majembe kuelekea mashambani. Imani yao huwa, **achanikaye kwenye mpini hafi njaa.** Wapo wachuuzi wanaosukuma mikokoteni yenye madebe ya maziwa ya kuuza. Wapo wanaoenda kufanya kazi kwenye majengo na viwanda. Wengine wamevaa suti na tai, wanaelekea afisini au shuleni kufundisha. Vilevile, wapo wanafunzi wanaoelekea shuleni na vyuoni. Hakika, kila mja katika kijiji hiki hushughulika.

Bidii ya wakazi wa Fanaka imewawezesha kujitegemea. Fanaka haijawahi kukosa chakula. Japo mvua hainyeshi kila msimu, maghala ya wenyeji huwa yamejaa chakula. Ukiwauliza vipi wanaweza kuwa na chakula kila msimu, wao hukuambia kuwa ukame haumzuii mtu kuilisha familia yake. Wao wamechimba visima vya maji. Wananyunyizia mimea yao maji. Hii ndiyo maana kijiji cha Fanaka kinavipatia vijiji vingine chakula.

6. Ni jibu lipi sahihi kulingana na **aya ya kwanza**?
   A. Kaskazini mwa Kaunti ya Kambini mna vijiji vitano.
   B. Eneo la Jitegemee ndilo dogo zaidi katika Kaunti ya Kambini.
   C. Sehemu nyingi katika Kaunti ya Kambini huwafurahisha wengi.
   D. Kaunti ya Kambini husifiwa na wenyeji wengi.

7. Kifungu kinaonyesha kwamba wanakijiji wa Fanaka wana bidii kwani:
   A. Anayezuru kijiji hicho hukutana na watu wengi.
   B. Hakuna yeyote katika kijiji hiki asiyekuwa na kazi ya kufanya.
   C. Wanakijiji huendeleza shughuli zao kwa kuaminiana.
   D. Watu wanafanya kazi viwandani bila kuona ugumu.

8. Kama ungeishi katika kijiji cha Fanaka, ungepata faida gani?
   A. Kujenga majengo ya fahari.
   B. Kuwauzia wakaazi wa vijiji vingine chakula.
   C. Kupata riziki kwa urahisi.
   D. Kujifunza ushirikiano katika utendakazi.

**Swali la 9 hadi la 12**

*Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.*

**Adili:** (*Akimtazama Kasimu*) Hujambo kaka? Naona leo umefika mapema mno. Kuna nini?

**Kasimu:** (*Akimwonyesha sare ambayo amevaa*) Jamani! Mtu akikusikia atadhani mimi hufika hapa saa tano! Je, umesahau leo ni Ijumaa ?

**Adili:** Nitasahau vipi na leo ni siku ya gwaride?

**Kasimu:** Ndiyo, leo kuna gwaride. Unajua kikundi chetu cha wanaskauti ndicho kinachoongoza. Nataka wenzangu wakija wanipate hapa. Tutafanya mazoezi kwanza. Staki aibu.

**Adili:** Kumbe! Nilikuwa nimesahau kuwa wewe ndiye kiongozi.

**Kasimu:** Na kiongozi mara zote …

**Adili:** Huongoza akina Adili wakimfuata.

**Kasimu:** Adili nawe, huachi utani?

**Adili:** Utani? Kwani kiongozi hufanya nini? Hukumbuki ulichotuambia Alhamisi?

**Kasimu**: Alhamisi gani?

**Adili:** Kwani kuna Alhamisi ngapi? Alhamisi si ni hiyo hiyo moja?

**Kasimu:** Ndiyo, ni moja, ila ni nyingi tu.

**Adili**: Kasimu. Huachi kuutia ubongo wangu katika mtihani. Itakuwaje moja na wakati huo huo ziwe nyingi?

**Kasimu**: Sidhani ni mtihani. Huoni kwamba kila wiki huwa na Alhamisi tofauti na ya wiki nyingine?

**Adili**: Oh! Kweli. Naona umekuwa kiongozi kweli kweli. **Mlezi wangu huniambia kwamba kiongozi sharti awaelimishe anaowaongoza.** Naona ukiendelea hivyo **tutakuteua** kuwa Kiranja Mkuu.

**Kasimu**: Wakati wa kuwa Kiranja Mkuu utafika. Ila tulikuwa tunazungumzia Alhamisi. Niliwaambia nini?

**Adili**: Umesahau? Basi Alhamisi ya mwanzo wa mwezi huu tulikuwa na kikao cha kusoma kitabu kitakatifu huko nyumbani. Wewe ndiye uliyekuwa unaongoza kikao. Ulitusomea aya kuhusu kiongozi mwema. Ulituambia kuwa kiongozi sharti awe mfano mwema kwa wengine. Aidha ulitueleza kwamba kiongozi lazima atekeleze majukumu yake ipasavyo.

**Kasimu**: Nakumbuka.

**Adili**: Ni hivyo, mwenzangu. Kiongozi lazima awe mwangalifu siku zote asiwapotoshe wengine. Jitazame ulivyo leo. Sare yako ni nadhifu mno. Je, wenzako kweli watavaa nguo chafu?

**Kasimu:** Bila shaka watajaribu kuwa nadhifu. Hata naona mmoja wao ndiye huyo. Acha tuwahi mazoezi. Akina Adili wanahitaji kuonyeshwa njia bora ya kupiga saluti. (A*naondoka huku akichekacheka)*

**Adili:** *(Akipaza sauti)* Haya, haya kiongozi bora. Tuonane baadaye.

9. Kwa nini Kasimu alifika shuleni mapema siku hiyo?
   A. Ni mazoea yake kufika mapema kila siku.
   B. Ni mwanachama wa kikundi cha wanaskauti.
   C. Ilikuwa siku ya gwaride shuleni mwao.
   D. Kikundi cha wanaskauti hakipendi aibu.

10. ‘‘Mlezi wangu huniambia kwamba kiongozi sharti awaelimishe anaowaongoza.’’
    Sentensi hii imetumika katika kifungu kuonyesha kwamba:
    A. Wanaoongozwa lazima wawaelekeze wengine.
    B. Wazazi wanawafahamu viongozi wote wema.
    C. Familia huwashauri watoto kuhusu uongozi.
    D. Watoto humtegemea kiongozi kwa kila jambo.


11. Fikiria kwamba leo ni Jumatatu. Darasa la akina Kasimu lina kikao cha mjadala kesho kutwa. Je, mjadala utafanywa siku gani?
    A. Jumatano
    B. Jumanne
    C. Alhamisi
    D. Ijumaa

12. Maana ya **tutakuteua** kulingana na kifungu ni :
    A. tutakuchagua
    B. tutakuamini
    C. tutakushauri
    D. tutakuomba

**Swali la 13 hadi la 15**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*



Juma, Maria, Asha, Yohane na Teresia walimtembelea nyanya yao kijijini. Nyanya hutengeneza mikeka, vikapu na fagio. Yeye hutumia vifaa hivi nyumbani na vingine huvipeleka sokoni kuviuza.

Vijana hawa walimsaidia nyanya yao katika shughuli hiyo. Juma, Maria na Teresia walifuma mikeka. Maria, Yohane na Teresia walitengeneza fagio. Wote, isipokuwa Juma na Teresia walifuma vikapu. Wavulana wote walileta vifaa vya kufanyia kazi. Baada ya kumaliza kazi, vijana wote isipokuwa Asha walifagia eneo walilofanyia kazi. Vijana wote isipokuwa Maria walimsaidia nyanya kupeleka bidhaa walizotengeneza sokoni.

13. Ni kijana yupi alitengeneza vifaa vitatu?
    - A. Asha
    - B. Yohane
    - C. Maria
    - D. Juma

14. Ni nani **hakumsaidia** nyanya kupeleka bidhaa sokoni?
    - A. Teresia
    - B. Maria
    - C. Yohane
    - D. Juma

15. Kulingana na kifungu:
    - A. Yohane, Maria na Asha walifuma vikapu.
    - B. Teresia, Yohane na Juma walifuma mikeka.
    - C. Asha, Maria na Teresia walifuma mikeka.
    - D. Juma, Maria na Yohane walifuma vikapu.

**Swali la 16 hadi la 20**

*Soma kifungu kifuatacho. Kwa kila swali umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo* ***zaidi*** *kati ya yale uliyopewa.*


Kedi aliishi katika nyumba _16_. Kwenye sakafu _17_ nyumba hiyo kulikuwa na _18_ maridadi. Pia kulikuwa na makochi ya kukalia. Vitu hivi viliifanya nyumba _19_. Kila siku Kedi _20_ kupiga deki sakafu ili kuondoa vumbi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 16. | A. nzuri | B. kuzuri | C. vizuri | D. mzuri |
| 17. | A. kwa | B. mwa | C. ya | D. la |
| 18. | A. fremu | B. pazia | C. kizingiti | D. zulia |
| 19. | A. kupendea | B. kupendeza | C. kupendezwa | D. kupendezana |
| 20. | A. amefurahia | B. atafurahia | C. alifurahia | D. akifurahia |

**Swali la 21 hadi la 30**

*Chagua jibu sahihi.*

21. Hii ni picha ya kifaa cha nyumbani.



Chagua sauti zinazokamilisha jina la kifaa hicho.

**b_l_uri**

A. i, a
B. u, i
C. o, a
D. e, i

22. Hili ni jedwali la maneno. Chagua jibu linaloonyesha vitendo?

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | pika | nunua | saidia |
| B | heshima | sahani | kifutio |
| C | bora | tulivu | nyingi |
| D | haraka | kabisa | sana |

23. Maneno haya yanavyofuatana vipi katika kamusi?
i. pera
ii. papai
iii. pesheni
iv. parachichi

A. (iv), (i), (iii), (ii)
B. (ii), (iv), (i) (iii)
C. (iv), (iii), (ii), (i)
D. (ii), (i), (iv), (iii)

24. Yafuatayo ni majina ya vifaa vinavyopatikana shuleni. Ni yapi yaliyo katika ngeli moja?
A. rula, chati, bendera
B. kalamu, uwanja, kabati
C. ubao, rafu, mlingoti
D. wino, dawati, penseli

25. Chagua jibu ambalo ni wingi wa sentensi:
Mkoba wa mwanafunzi una kitabu.
A. Mikoba ya mwanafunzi ina kitabu.
B. Mikoba ya wanafunzi ina vitabu.
C. Mikoba ya wanafunzi ina kitabu.
D. Mikoba ya mwanafunzi ina vitabu.

26. Chagua jibu ambalo lina maneno ambayo ni kinyume.
A. mgeni – mwenyeji
B. mzazi – mlezi
C. nyanya – ajuza
D. kaka – ndugu

27. Chagua jibu linalounganisha sentensi hizi kwa usahihi.
i) Tina alimpikia Saimo chai.
ii) Saimo alimpikia Tina chai.

A. Saimo alipikiwa chai kwa Tina.
B. Tina alipikia chai kwa Saimo.
C. Tina na Saimo walipikiana chai.
D. Saimo na Tina walipikiwa chai.

28. Chagua sentensi ambayo ni ukanusho wa:
Wachezaji wataimba wimbo wa taifa.
A. Wachezaji hawakuimba wimbo wa taifa.
B. Wachezaji hawangeimba wimbo wa taifa.
C. Wachezaji hawajaimba wimbo wa taifa.
D. Wachezaji hawataimba wimbo wa taifa

29. Ni sentensi ipi iliyo katika hali ya udogo?
A. Kijito hicho kina maji safi.
B. Kiwiko cha mkono wake kimepona.
C. Kiberiti kimenunuliwa na mama.
D. Kiota cha ndege kinavutia.

30. Chagua jibu lenye maana sahihi ya nahau.
A. piga hatua – angalia mbele ili usianguke.
B. piga hodi – subiri mlangoni ili kufunguliwa.
C. fanya haki – kumpa mtu anachostahili kupata
D. fanya bidii – endelea na shughuli fulani kwa kasi.

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**